-pJINA ……NAMBARI …….SAHIHI ……

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI YA KISWAHILI

MACHI / APRILI 2017

MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE 2017

CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI KENYA

MAAGIZO

a. Jibu maswali MANNE pekee.

b. Swali la kwanza ni la LAZIMA

c. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Tamthlia, Riwaya ,Ushairi, na Hadithi Fupi.

d. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

SWALI LA LAZIMA

1.(a)(i) Ni nini maana ya maghani? (alama 2)

(ii) Eleza sifa **nne** za maghani. (alama 8)

(b)(i) Eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(ii) Fafanua dhima **nne** za vitanza ndimi katika jamii. (alama 8)

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

T. Arege: *Mstahiki Meya*

Jibu swali la 2 au la 3.

2. “Si habari za kwenda nyumbani! Nimeona niache hii kazi….”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua sababu **tano** za mnenaji kuacha kazi.(alama 10)
c) Eleza sifa na umuhimu wa mnenewa. (alama 6)

3. Tamthilia ya **Mstahiki Meya** inasawiri picha halisi ya mataifa mengi barani Afrika. Dhihirisha. (al.20)

SEHEMU YA C : RIWAYA

K. Walibora : *Kidagaa Kimemwozea*

Jibu swali la 4 au la 5.

4. Mwanamke amesawiriwa vipi katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea? (al 20)

5. ‘ …Ila kumbuka kwamba wengine sisi hatuna asili wala fasili. Dunia imekhitari kutupuuza na kutudunisha tukawa si chochote si lolote.’

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha tamathali **tatu** za usemi zilizotumika katika dondoo hili. (alama 6)
c) Mnenaji ni msiri kama kaburi. Thibitisha kwa mujibu wa riwaya nzima. (al 7)
d) Mnenewa ni mwanamapinduzi. Thibitisha. (alama 3).

SEHEMU YA D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. **ULIYATAKA MWENYEWE**:

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,

Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo ! hutaki,

Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,

Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,

Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,

Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,

Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,

Mishikeli mia mia, kwako ona haitoki,

Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,

Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,

Ulimwengu ni shujaa, hilo kama hukumbuki,

Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,

Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,

Ulijidhania simba, hutishiki na fataki,

Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,

Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,

Na tena ukajiona,kwambawe mstahiki,

Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,

Uliyataka mwenyewe!

Majuto ni mjukuu, huja kinyume rafiki,

Ungejua mwisho huu, ungetenda yalo haki,

Uko roho juu juu,popote hapakuweki,

Uliyataka mwenyewe!

Maswali

(a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)

(b) Tambua jinsi <u>mbili</u> anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (alama 2)

(c) Taja na utoe mifano ya aina zozote <u>mbili</u> za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (alama 4)

(d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari. (alama 4)

(e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina <u>mbili</u> za idhini ya kishairi katika

shairi hili. (alama 4)

(f) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)

(i) Mstahiki

(ii) Hupuliki

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1.Lau tungekuwa sawa,
Na wizi haungekuwako,
Kufuli hazingetengenezwa,
Komeo na kadhalika.

2.Lau tungekuwa sawa,
Hakungekuwa sheria,
Sheria aina aina,
Za Mungu na bin – Adamu.

3.Lau tungekuwa sawa,
Wanyonge hawangekuwako,
Matajiri vilevile,
Na watu hawangeshindana.

4.Lau tungekuwa sawa,
Njaa haingekuwako,
Ila shibe na nyemi,
Maisha ya kutaanasi.

5.Wagonjwa wasingekuwako,
Madawa hayangetengenezwa,
Madaktari na wengineo,
Wote hawangekuweko.

6.Wajinga wasingekuwako,
Werevu ni vilevile,
Ndio kukawa wanafu,
Pamoja na wakufunzi.

7.Ujana ‘singekuwako,
Uzee ungeingiaje?
‘Singekuwako watawaliwa,
Utawala ungekwisha.

8.Isingekuwa uovu,
Uovu wa bin – Adamu,
Hatungenyimana haki,
Uhalifu ungekwisha.

Maswali

a)Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alama 3)

a) Taja matokeo **manne** ya kukosekana kwa usawa. (alama 4)
b) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)
c) Kwa kutoa mifano miwili tambua mbinu moja ya uhuru wa kishairi iliyotumika shairini. (alama 3)
d) Takriri imetumika vipi katika shairi hili? (alama 3)
e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi:

i) Sawa ii) komeo iii) kutaanasi (alama 3)

SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

K. Walibora na S. A. Mohamed (wah): *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

8. " …Niliipita sebule na kufululiza hadi kwenye chumba cha malazi. Mlangoni nilikaribishwa na harufu ya manukato iliyozidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia…."

a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Kwa kuirejelea hadithi nzima onyesha ufaafu wa anwani ya hadithi hii. (alama 16)